



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE
KATIKA MAJIMBO MATATU NA UDIWANI KATIKA
KATA MBILI - TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Ubunge katika Majimbo matatu, Jimbo la Korogwe Vijijini, Mkoa wa Tanga kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo **Ndugu Stephen Hilary Ngonyani**, Jimbo la Ukonga katika Mkoa wa Dar Es Salaam na Jimbo la Monduli katika Mkoa wa Arusha, kufutia waliokuwa Wabunge wa Majimbo hayo **Ndugu Mwita Mwikabe Waitara** na **Ndugu Julius Kalanga Laizer** kujiuzulu uanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na hivyo kupoteza sifa za kuwa Wabunge.

Baada ya kupokea taarifa hizo na kwa mujibu wa vifungu vya 37 (1) (b) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuwa majimbo matatu ya **Korogwe Vijijini, Ukonga na Monduli yapo wazi.**

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 37(1)(b) (5) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Tume inatoa taarifa wa Umma kuhusu Ratiba ya uchaguzi mdogo katika majimbo hayo kama ifuatavyo:

1. **Fomu za Uteuzi** katika Majimbo hayo zitatolewa kuanzia tarehe 13 hadi 20 Agosti, mwaka huu.
2. **Uteuzi wa Wagombea** utafanyika tarehe 20 Agosti, mwaka huu.
3. **Kampeni za Uchaguzi** zitaanza tarehe 21 Agosti, na kumalizika tarehe 15 Septemba, mwaka huu.
4. **Siku ya uchaguzi** itakuwa tarehe 16 Septemba, mwaka huu.

Tume pia inatoa taarifa kwa umma kuwa uteuzi, Kampeni na uchaguzi wa Madiwani kwa Kata za Tindabuligi na Kisesa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu uliohirishwa hapo awali utafanyika sambamba na ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa ubunge katika Majimbo hayo matatu.

Tume inachukua nafasi hii kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maelekezo yote wakati wa kipindi cha uchaguzi mdogo wa Majimbo hayo matatu na hizo Kata mbili.

Imetolewa leo tarehe 04 Agosti, 2018 na;



Mhe. Jaji (R) Mbarouk Salim Mbarouk

MAKAMU MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI